

I Idara ya Elimu ya NSW

Ushauri uliosasisha wa COVID-19

[Idara ya Afya ya NSW](#) ilitoa ushauri mpya wa COVID-19 kwa shule tarehe 14 Agosti 2020. Huu unabadilisha jinsi shule zetu zinavyofanya kazi.

1. Watoto ambao ni wagonjwa wenye dalili kama za homa ya mafua, hata ikiwa ni dalili kidogo, wanapaswa kukaa nyumbani. Watoto ambao wanakuwa wagonjwa shuleni watakaa kwenye chumba cha wagonjwa na mipango itafanywa ili watachukuliwa.
 - Idara ya Afya ya NSW imeomba kuwa shule zitie moyo mtu yeyote ambaye hajisikii vizuri au ana dalili kidogo kama za homa ya mafua, kupanga kupimwa kupitia mtaalamu wao wa matibabu au mojawapo ya [zahanati ya COVID-19](#).
 - Wanafunzi na wafanyakazi walio na dalili kama za homa ya mafua watahitaji kutoa nakala ya matokeo ya kipimo cha COVID-19 yanayoonyesha hana kabla ya kuruhusiwa kurudi shuleni.
2. Inapowezekana, wanafunzi watakaa ndani ya kikundi chao (k.m. darasa, kikundi cha mwaka, au hatua) kwa shughuli zote za kujifunza ndani ya shule zao ili kupunguza mawasiliano ya karibu.
3. Matembezi yasiyo muhimu kwa shule haziruhusiwi. Ikiwa unataka kuongea na mwalimu au mfanyakazi wa shuleni, unapaswa kupiga simu shuleni na kupanga mkutano. Mkutano utakuwa ama kwa simu au kupitia mkutano wa video.
4. Shughuli kati za shule zinapaswa kuwepo ndani ya jamii au eneo la mtaa. Kanivali za michezo au shughuli zinazofanana na mikusanyiko mikubwa ambapo zaidi ya shule mbili zinahusika hairuhusiwi.
5. Kuimba kwa vikundi vyote (kwaya) na/au shughuli zingine za kuimba, na pia matumizi ya vyombo vya upepo katika mahali pa kikundi, hairuhusiwi. Mipangilio maalum iko kwa wanafunzi wa Cheti cha Shule ya Juu (HSC).
6. Wanafunzi wa Year 11 na Year 12 wanaomaliza masomo (HSC) wanaweza kuendelea kuhudhuria masomo/shughuli zinazohusiana na masomo yanayopatikana tu kwenye kampasi nyingine. Wanafunzi wengine wote ikiwa ni pamoja na wanafunzi wa Year 11 ambao hawatamaliza somo la HSC wasihudhurie kampasi nyingine kwa muda uliobaki ya Term 3. TAFE na programu zingine za VET zinaweza kuendelea.

Ingawa mwelekeo wa shule ya chekechea ya 2021 imesalia, kuna maoni ya kusaidia yanayopatikana kupitia [department's website](#) (tovuti ya idara). Mapendekezo haya yatasaidia kuweka wanafunzi msisimko na kushiriki kwa mabadiliko yao kwa chekechea.

Panga mkutano na shule yako ili kujua zaidi kuhusu mabadiliko hayo.

Huduma ya Ukalimani wa Simu

Ikiwa unahitaji habari zaidi tafadhali piga simu kwa mwalimu mkuu wa shule yako. Ikiwa unahitaji mkalimani kukusaidia kwa maswali yako tafadhali piga simu kwa Huduma ya Ukalimani wa Simu kwenye 131 450 na uombe mkalimani kwa lugha yako. Huduma hii itakuwa ya bure kwako.